# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

**Mtaa wa Nkoani,**
**S.L.P 273,**
**55103 RUKWA,**
**Barua pepe: rbcrukwa@pccb.go.tz.**
**TANZANIA.**

**Tovuti: www.pccb.go.tz**

# TAARIFA KWA UMMA

## TAARIFA YA UTENDAJI KAZI MWEZI JANAURI HADI MACHI, 2020 -TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA MKOA WA RUKWA

**RUKWA APRILI 24, 2020**

**Ndugu waandishi wa habari,**
Tunapenda kuwajulisha wananchi wa mkoa wa Rukwa kwamba, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Rukwa imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kazi kwa kushirikiana na ofisi zake zote za wilaya na wananchi kwa ujumla, ambapo kwa robo ya tatu ya mwaka (mwezi Janauri hadi Machi, 2020) imetekeleza mambo yafuatayo katika eneo la uchunguzi na mashtaka, ukaguzi wa miradi ya maendeleo na uelimishaji umma.

### 1. Uchunguzi na Mashtaka

Katika kipindi hiki tulipokea jumla ya taarifa 24 ambapo kati ya hizo, taarifa 05 zilitoka Halmashauri ya Manispaa, taarifa 04 zilitoka Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga, taarifa 09 zilitoka Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo na taarifa 05 zilitoka Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi. Taarifa zote hizi zipo katika hatua mbalimbali za kiuchunguzi.

**Ndugu waandishi wa habari,**
Pamoja na takwimu hizo hapo juu, naomba nitoe ufafanuzi kuhusu tuhuma za rushwa na utapeli unaofanywa na wakopeshaji haramu, ufafanuzi kuhusu udhibiti wa mapato ya serikali katika Halmashauri za Wilaya na ufafanuzi kuhusu ubadhirifu wa fedha katika vyama vya ushirika (Saccos) Mkoa wa Rukwa.

### 1.1. Uchunguzi juu ya tuhuma za rushwa na utapeli unaofanywa na wakopeshaji haramu.

**Ndugu waandishi wa habari,**
Katika kuendeleza mapambano dhidi ya wakopeshaji haramu ambao wanatapeli watu na kuinyima serikali mapato, mnamo mwezi Februari, 2020 ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Rukwa ilipokea taarifa kutoka kwa msiri kwamba ndugu Lenatus Damiano Pempula mkazi wa Sumbawanga mjini amekuwa akifanya biashara haramu ya ukopeshaji fedha kwa riba kubwa kwa watu mbalimbali ndani ya mkoa wa Rukwa, wengi wao wakiwa ni watumishi wa umma hasa wastaafu bila kusajiliwa wala kulipia kodi za Serikali.

Baada ya kupata taarifa hiyo tulianzisha uchunguzi na moja ya hatua za awali tulizochukua tulimkamata mtuhumiwa na kumfanyia upekuzi nyumbani kwake ambapo tulifanikiwa kupata vielelezo mbalimbali yakiwemo madaftari anayotumia kuwaandikisha madeni feki wakopaji wake.

Pia tulipata nyaraka mbalimbali za miamala ya benki pamoja na kadi 85 za ATM zikiwemo kadi 57 za benki ya NMB, kadi 15 za benki ya CRDB, kadi 12 za benki ya POSTA na kadi 1 ya benki ya NBC za waathirika 75 tofauti ambazo mtuhumiwa alizishikilia kama dhamana ya madeni yake na kuzitumia kutoa fedha benki katika akaunti za waathirika hao.



Mpaka sasa tumefanikiwa kuwapata waathirika 27 waliotapeliwa ambao kwa ujumla wao walikopeshwa na mtuhumiwa jumla ya Tsh 24,205,000/= kwa vipindi tofauti toka mwaka 2011 mpaka mwezi Januari mwaka huu 2020 na kwamba kwa ujumla wao wamekwisha mlipa mtuhumiwa jumla ya Shilingi 349,782,478/= kiasi ambacho kwa lugha rahisi ni sawa na asilimia 1,445 ya mkopo waliopatiwa.

TAKUKURU mkoa wa Rukwa imefanya utaratibu wa kuwawezesha waathirika waliotapeliwa kuweza kuendelea kuchukua fedha zao za mishahara na pensheni zao za mwezi katika akaunti zao pasipo kuingiliwa na mtuhumiwa.

Tunaendelea na juhudi za kuwatafuta waathirika wengine 48 ambao kadi zao zilikutwa kwa mtuhumiwa ili tukamilishe uchunguzi huu.Tunatoa wito kwa waathirika hao wafike ofisini ili wasaidiwe.

Vilevile TAKUKURU Mkoa wa Rukwa inatoa onyo kwa wakopeshaji wote wa aina hii kuacha mara moja kwani watakapobainika hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

### 1.2. Ubadhirifu wa fedha katika vyama vya ushirika:

**Ndugu waandishi wa habari,**
Katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka mwezi Oktoba hadi Desemba, 2019 tuliwaambia kwamba tumewakamata viongozi wa Nkasi Teacher`s Saccos wilayani Nkasi baada ya kuandaa mkopo hewa wa Shilingi 55,000,000/= ambazo ni mali ya wanachama wa Saccos hiyo na haikujulikana fedha hizi walimkopesha nani, kama tulivyowaeleza katika taarifa hiyo tulifanikiwa kuwakamata viongozi hawa na kuwataka warejeshe fedha hizi ndani ya siku 14.

**Ndugu waandishi wa habari,**
Mpaka kufikia robo ya tatu ya mwaka mwezi Januari hadi Machi, 2020 viongozi hawa wamerejesha kiasi cha shs. 39,265,000/=, aidha bado tunaendelea kuwabana ili warejeshe fedha yote iliyosalia shs. 15,735,000/=, tunatarajia kuikabidhi fedha hii kwa wanachama mara itakapokamilika.

### 1.3. Uokoaji wa fedha za Halmashauri za wilaya Mkoa wa Rukwa:

Ili kudhibiti upoteaji wa mapato ya serikali katika Halmashauri za wilaya mkoa wa Rukwa, katika kipindi cha mwezi Januari hadi Machi, 2020, TAKUKURU Mkoa wa Rukwa tumefanikiwa kuokoa jumla ya fedha shs. 10,880,000/= kutoka kwa wadaiwa sugu (watendaji wa vijiji) wa ukusanyaji mapato kwa njia ya POS katika Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo, ambapo kijiji cha Kizombwe tumeokoa shs. 520,000/=, kijiji cha Kalembe tumeokoa shs. 3,100,000/= kijiji cha Sopa tumeokoa shs. 4,460,000/= na kijiji cha Mkowe tumeokoa shs. 2,700,000/=; bado tunaendelea na zoezi hili ili kuhakikisha wadaiwa wote sugu wanawasilisha fedha walizokusanya katika Halmashauri za wilaya.

## 2. Ukaguzi wa miradi ya maendeleo

**Ndugu waandishi wa habari,**
Katika kipindi cha mwezi Januari hadi Machi, 2020, tumefanya ukaguzi wa mradi wa ujenzi wa barabara ya lami yenye umbali wa kilimita 2 kijiji cha Matai Wilaya ya Kalambo uliyokuwa unatekelezwa na Mkandarasi wa Kampuni ya GRAND TECH (T) Limited ya Dar es Salaam baada ya kuingia Mkataba na Mratibu wa TARURA Mkoa wa Rukwa tarehe 04/03/2019 kwa gharama ya tshs. 899,755,000/=, mkandarasi alipaswa kuanza kazi hii tarehe 19/03/2019 na kukamilisha tarehe 19/07/2019. Katika ukaguzi tuliyofanya, tulibaini kwamba Mkandarasi hakukamilisha kazi ndani ya kipindi cha mkataba na aliomba muda wa nyongeza ambapo alipewa muda mpaka tarehe 02/11/2019 ili amalize kazi hii, lakini hata ulipofika muda huo wa nyongeza Mkandarasi alikuwa hajamaliza kazi na kuikabidhi kwa mwajiri (TARURA Wilaya ya Kalambo).

Kupitia maombi ya malipo ya sh. 121,584,828.44 ya mkandarasi katika *Interim Payment Certificate No. 05*, Mwajiri (TARURA) alimkata Mkandarasi *Liquidated Damage* ya tsh. 53,985,300,/= kati ya fedha hizo alizoomba kwa usimamizi wa TAKUKURU ambayo ni makato ya kuanzia tarehe 01/11/2019 hadi 01/01/2020 ambayo ni sawa na 0.1% ya gharama za mradi.



## 3. Elimu Kwa Umma

**Ndugu waandishi wa habari,**
Ni wajibu wetu kushirikisha umma katika juhudi za kuzuia na kupambana na rushwa kupitia mikutano ya hadhara, semina, vipindi vya redio pamoja na maonesho, ambapo watu wa kada na rika mbalimbali katika kipindi hiki wameelimishwa hasa katika maeneo ya kukataa na kutoa taarifa dhidi ya vitendo vya rushwa ya ngono na elimu ya madhara ya rushwa katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Vilivile tumewaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kukataa na kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kupitia Kampeni ya UTATU, matumizi ya TAKUKURU APP na Vunja Ukimya Kataa Rushwa ya Ngono.

Kabla ya kufungwa kwa shule na vyuo tuliimarisha klabu 86 za wapinga rushwa katika shule za msingi na sekondari. Tulifanya hivi kwa kuamini kwamba vijana ni jeshi muhimu sana katika kufanikisha mapambano dhidi ya rushwa.

Mwezi Februari, 2020, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ilizindua Mkakati rasmi wa kushirikiana na vijana wa Skauti katika kuzuia na kupambana na rushwa nchini, uzinduzi huu ulifanywa na Makamu wa Rasi katika mkoa wa Dodoma.

Uelimishaji uliofanyika umechangia kupokelewa kwa taarifa nyingi za vitendo vya rushwa na makosa yahusianayo na rushwa, ni vyema kwamba viongozi na watumishi wa maeneo yanayoonekana kuongoza kwa kulalamikiwa kujihusisha na vitendo vya rushwa wachukue hatua mapema ikiwa ni pamoja na kuimarisha mikakati yao ya ndani ya kudhibiti rushwa.

**Ndugu waandishi wa habari,**
Katika robo ya Aprili hadi Juni, 2020 TAKUKURU Mkoa wa Rukwa itaendelea kuwahamasisha wananchi kushiriki kivitendo katika kuzuia rushwa na tutaendelea kutoa elimu ya rushwa kuelekea kwenye uchaguzi. Aidha tutaendelea kufuatilia madeni ya vyama vya ushirika na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuhakikisha kwamba miradi inayotekelezwa na wakandarasi inalingana na thamani halisi ya fedha iliyotolewa na serikali (value for money).

**Wito:**

**Ndugu Wanahabari,**
Tukumbuke kwamba mwaka huu wa 2020 ni mwaka wa Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani, TAKUKURU tunaendelea kupokea taarifa za vitendo vya rushwa ambavyo vinafanywa na baadhi ya wananachama wanaowania nafasi mbalimbali za uongozi katika uchaguzi ujao, ni vema wananchi hawa wanaonyemelea majimbo na kata mbalimbali wakaheshimu sheria, kanuni na taratibu za uchaguzi.

TAKUKURU inawataka wanasiasa wote wanaomba uongozi mbalimbali wa vyama kutoa ushirikiano wa dhati TAKUKURU inapohughulikia rushwa kwenye uchaguzi na wajiepushe na rushwa na yale yanayokatazwa na sheria za uchaguzi kwani mwisho wa siku vitendo hivi vitawagharimu.

Ninatambua na kuthamini sana mchango wa vyombo vya habari katika mkoa wetu wa Rukwa kwani siku zote mmekuwa mstari wa mbele kutoa fursa za uelimishaji dhidi ya rushwa na pia kuuhabarisha umma juu ya jitihada zinazofanywa na serikali katika kuzuia na kupambana na rushwa ndani ya mkoa wetu. Naomba tuendelee na moyo huo wa kizalendo.

**Imetolewa na:**
**HAMZA MWENDA**
**MKUU WA TAKUKURU (M) WA RUKWA**
**TAREHE: 24/04/2020**

*Barua zote zitumwe kwa Mkuu wa Takukuru Mkoa , Mtaa wa Mkoani, S.L.P 273, 55103 SUMBAWANGA. Unaweza pia kuwasiliana nasi kwa njia ya simu ya Bure 113,* ***instagram****: takukuru.tz,* ***Facebook****: TakukuruTz,* ***Twitter****:TAKUKURU.TZ,*

***OnlineTV,*** *TAKUKURUTV.*